# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## KIKAO CHA KWANZA

**29 AGOSTI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 29 AGOSTI, 2023

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA:**

**III. TAARIFA YA SPIKA:**

**IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023].*

## V. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**1. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mkuu:-

Je, nini mpango wa Serikali kuhusu malalamiko ya Wastaafu juu ya Kikokotoo kinachotumika kupiga mahesabu na kulipa mafao.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**2. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Kizazi - Kibondo.

**3. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Soko na Stendi ya kisasa eneo la Njiapanda Merya Halmashauri ya Wilaya Singida.

**4. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu kadhia ya maji yanayotuama maeneo mengi wakati wa mvua katika Jiji la Dar es Salaam.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**5. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, ni fursa gani za uwekezaji zinapatikana Tanzania.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**6. MHESHIMIWA DKT CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Gairo hadi Nongwe itajengwa kwa kiwango cha lami.

**7. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini *TANROADS* Mkoa wa Mara wataondoa vigingi katika maeneo ya Wananchi baada ya kushindwa kulipa fidia.

## WIZARA YA NISHATI:

**8. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Ofisi ya Wilaya ya *TANESCO* – Kibiti.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**9. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Kitulo.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**10. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini kumekuwa na ugumu wa upatikanaji mikopo kwa Wanafunzi waliosoma Shule za Binafsi wanapojiunga na elimu ya juu.

**11. MHESHIMIWA NORAH WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la uhaba wa Hosteli kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu wanaosoma katika Vyuo vya Mkoa wa Morogoro.

## WIZARA YA MADINI:

**12. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali itawasaidia Wanawake na Vijana wa Kata za Mitesa na Nanjota wanaojihusisha na uchimbaji Madini Lulindi.

## WIZARA YA KILIMO:

**13. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua changamoto za Wakulima waliowekeza kwenye *SACCOS* na fedha zao kupotea.

**14. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini kutakuwa na Kiuatilifu kimoja cha magonjwa kwenye Zao la Korosho.

## WIZARA YA FEDHA:

### 15. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, hesabu zinazowasilishwa na CAG kila Mwaka ni za mashaka au za uhakika.

### 16. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na nchi jirani za Afrika Mashariki.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 17. MHESHIMIWA TAMIMA HAJI ABASS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati nyumba za makazi ya Askari Polisi Kaskazini Unguja.

**18. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kufanya mazoezi ya utayari katika uokozi wa ajali majini katika Kivuko cha Kivukoni-Kigamboni.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**19. MHESHIMIWA SANTIEL ERIC KIRUMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali haioni haja ya kuhimiza Mashirika mengine ya Simu kujiunga na Mpango wa M-Mama kwani umekuwa msaada kwa Wajawazito wengi.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**20. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga Mnada wa Kimataifa wa Mifugo katika kijiji cha Mwandoya.

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2023 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2023].*

**DODOMA**
**29 AGOSTI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**